

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**TAARIFA YA MAPOKEZI YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU
MWAKA 2017 KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**



“SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA NCHI YETU”

IMEANDALIWA NA:
MKUU WA WILAYA
S.L.P. 1070
LINDI


MEI 22, 2017

| | |
|--|-----------------------|
| <i>Yaliyomo</i> | <i>Ukurasa</i> |
| 1.0 PICHA ZA WAKIMBIZA MWENGE WA UHURU KITAIFA..... | 1 |
| 2.0 RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2017 | 2 |
| 3.0 UTANGULIZI..... | 5 |
| 4.0 ORODHA YA MIRADI YA MWENGE -2017..... | 6 |
| 4.1 TAARIFA YA MRADI WA UPIMAJI VIWANJA MAENEKO YA NGONGO NA NGURUMAHAMBA.... | 8 |
| 4.2 TAARIFA YA KIKUNDI CHA USINDIKAJI WA MAFUTA MWALI YA NAZI | 10 |
| 4.3 TAARIFA YA MRADI WA MATENGENEZYO YA BARABARA YA MTUTU-CHELEWENI | 12 |
| 4.4 TAARIFA YA UJENZI WA ZAHANATI YA NANDAMBI | 13 |
| 4.5 TAARIFA YA MRADI WA SHAMBA LA CHOROKO – CHIKONJI..... | 15 |
| 4.6 TAARIFA YA MRADI WA MAJI CHIKONJI | 17 |
| 4.7 TAARIFA YA UJENZI WA MADARASA 3 YA SHULE YA SEKONDARI MKONGE | 19 |
| 4.8 TAARIFA YA ASILIMIA 10 YA VIKUNDI YA WANAWAKE NA VIJANA..... | 20 |
| 4.9 TAARIFA YA MFUMO WA KIELEKTRONIKI KATIKA KITUO CHA AFYA MANISPAA YA LINDI..... | 22 |

1.0 PICHA ZA WAKIMBIZA MWENGE WA UHURU KITAIFA MWAKA 2017



Amour Hamad
Amour
(KIONGOZI)
KASKAZINI UNGUJA



Frederick Joseph
Ndahani
SINGIDA



Salome Obadia
Mwakitalima
KATAVI



Frederick Joseph
Ndahani
SINGIDA



Shukran Islam Msuri
MJINI MAGHARIBI



Bahati Mwaniguta
Lugodisha
GEITA

**2.0 RATIBA YA Mbio ZA MWENGE WA UHURU HALMASHAURI YA MANISPAA
YA LINDI TAREHE 22-23 MEI, 2017**

| TAREHE | MUDA | MAHALI | SHUGHULI | UMBALI (KM) | MHUSIKA |
|-----------|------------|-------------------------------------|--|-------------|-------------------------|
| 22/5/2017 | 12.30-2.30 | Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa | Msafara kuelekea eneo la mapokezi ya Mwenge S/M Mnazimmoja. | 25 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 2.30-3.30 | Kiwanja cha S/M Mnazimmoja | Kupokea Mwenge wa Uhuru | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 3.30-4.00 | Kiwanja cha S/M Mnazimmoja | KUTOA UJUMBE WA MWENGE | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 4.00-4.10 | Kiwanja cha S/M Mnazimmoja | Mwenge kuelekea eneo la Upimaji wa viwanja – NGONGO. | 7 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 4.10-4.15 | Eneo la Upimaji wa viwanja - NGONGO | Mwenge kuzindua mradi wa upimaji viwanja na kukabidhi Hati kwa ajiri ya Ujenzi wa Viwanda katika Maeneo ya Ngurumahamba. | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 4.15-4.20 | Eneo la Upimaji wa viwanja - NGONGO | Mwenge kuelekea Ngongo Sekondari | 1 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 4.20-5.00 | Shule ya Sekondari Ngongo | CHAI YA ASUBUHI | 0 | Mkurugenzi wa Manispaa |
| | 5.00-5.10 | Shule ya Sekondari Ngongo | Mwenge kuelekea Ng'apa | 10 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 5.10-5.25 | Ofisi ya Kata ya Ng'apa | Mwenge Kuzindua Mradi wa kukamua Mafuta ya Nazi na kukagua umaliziaji wa Ofisi ya Kata. | 0 | Mkuu wa Wilaya Ya Lindi |
| | 5.25-5.30 | Ofisi ya Kata ya Ng'apa | Mwenge kuelekea Cheleweni | 3 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 5.30-5.40 | Barabara ya Mtutu-Cheleweni | Mwenge kuweka jiwe la Uzinduzi wa Mradi. | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |

| TAREHE | MUDA | MAHALI | SHUGHULI | UMBALI (KM) | MHUSIKA |
|---------------|-------------|-----------------------------|---|--------------------|--------------------------|
| 22/5/2017 | 5.40-5.45 | Cheleweni | Mwenge kuelekea Nandambi | 8 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 5.45-6.05 | Zahanati ya Nandambi | Mwenge kufungua Zahanati. | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi. |
| | 6.05-6.15 | Zahanati ya Nandambi | Mwenge kuelekea Chikonji. | 12 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 6.15-6.30 | Shamba la Choroko | Mwenge kutembelea Shamba. | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 6.30-6.50 | Chikonji | Mwenge kuweka jiwe la msingi Mradi wa Maji. | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 6.50-7.00 | Chikonji | Mwenge kuelekea S/M Kineng'ene. | 10 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 7.00-8.00 | S/M Kineng'ene. | CHAKULA CHA MCHANNA | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 8.00-8.15 | S/M kineng'ene | Mwenge kuelekea Shule ya Sekondari Mkonge. | 15 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 8.15-8.30 | Shule ya Sekondari Mkonge | Mwenge kufungua Madarasa 3 na kukabidhi mifuko 100 ya Saruji kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Elimu Sekondari. | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 8.30-8.40 | Shule ya Sekondari Mkonge. | Mwenge kuelekea Wailes Majani Mapana | 3 | Mkurugenzi wa Manispaa |
| | 8.40-9.20 | Wailes Majani mapana | Mwenge kukabidhi Hundu za mikopo kwa Vikundi na kuona shughuli zinazofanywa na vikundi hivyo. | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 9.20-9.25 | Wailes Majani Mapana | Mwenge kuelekea kituo cha Afya cha Manispaa | 2 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 9.25-9.45 | Kituo cha Afya cha Manispaa | Mwenge kuzindua mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa shughuli za Afya (GoT – MIS), Kugawa kadi za CHF na kuona ukarabati wa kituo | 0 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |
| | 9.45-9.55 | Kituo cha Afya cha Manispaa | Kukimbiza Mwenge hadi Uwanja wa ILULU | 1 | Mkuu wa Wilaya ya Lindi |

| TAREHE | MUDA | MAHALI | SHUGHULI | UMBALI (KM) | MHUSIKA |
|--|-------------|---|--|--------------------|---------------------------------|
| 22/5/2017 | 9.55-11.00 | <i>Uwanja wa ILULU</i> | <i>Mwenge kukagua Mabanda ya Vita dhidi ya Rushwa, Madawa ya kulevyia na Mapambano Dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi na Malaria</i> | 0 | <i>Mkuu wa Wilaya ya Lindi.</i> |
| | 11.00-11.30 | <i>Uwanja wa llulu</i> | <i>Utambulisho</i> | 0 | <i>Mkuu wa Wilaya ya Lindi.</i> |
| | 11.30-12.00 | <i>Enaeo la Mkesha wa Mwenge Uwanja wa llulu</i> | <i>UJUMBE WA MWENGE</i> | 0 | <i>Mkuu wa Wilaya ya Lindi</i> |
| | 12.00-2.00 | <i>Enaeo la Mkesha wa Mwenge Uwanja wa llulu</i> | <i>Sanaa za Maonyesho , Burudani mbalimbali na Shamrashamra za Mwenge</i> | 0 | <i>Afisa Utamaduni Manispaa</i> |
| | 2.00-3.00 | <i>Ukumbi wa DDC</i> | <i>CHAKULA CHA JIONI</i> | 0 | <i>Mkurugenzi wa Manispaa</i> |
| | 3.00-11.30 | <i>Enaeo la Mkesha wa Mwenge Uwanja wa llulu</i> | <i>Sanaa za Maonyesho , Burudani mbalimbali na Shamrashamra za mkesha wa Mwenge</i> | 0 | <i>Afisa Utamaduni Manispaa</i> |
| 23/5/2017 | 11.30-1.30 | <i>Ukumbi wa DDC</i> | <i>CHAI YA ASUBUHI</i> | 0 | <i>Mkurugenzi wa Manispaa</i> |
| | 1.30-2.30 | <i>Enaeo la Mkesha wa Mwenge (Uwanja wa llulu)</i> | <i>Msafara wa Mwenge kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kuelekea kijiji cha Nanganga Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa</i> | 90 | <i>Mkuu wa Wilaya ya Lindi</i> |
| | 2.30-3.00 | <i>Kijiji cha Nanganga Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa</i> | <i>Kukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.</i> | 0 | <i>Mkuu wa Wilaya ya Lindi</i> |
| | 3.00-3.30 | <i>Kijiji cha Nanganga Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa</i> | <i>Msafara kutoka kijiji cha Nanganga Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa na kurudi Halmashauri ya Manispaa ya Lindi</i> | 90 | <i>Mkuu wa Wilaya ya Lindi</i> |
| MWENGE UTASAFIRI NDANI YA MANISPAA UMBALI WA KILOMITA | | | | 162 | |

3.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ni moja kati ya Halmashauri Sita za Mkoa wa Lindi na ndio Makao Makuu ya Wilaya na Mkoa wa Lindi. Manispaa ina ukubwa wa Kilomita za mraba 945 kati ya hizo, kilomita za mraba 833 ni eneo la nchi kavu na kilomita za mraba 112 ni eneo la Maji. Eneo linalofaa kwa kilimo ni Jumla ya Hekta 67,962 na eneo linalotumika kwa kilimo kwa mwaka ni Hekta 44,158 Aidha Hekta 835 zinatafaa kwa kilimo cha Umwagiliaji na eneo linalolimwa kwa umwagiliaji ni Hekta 442. Manispaa ya Lindi inapatikana kati ya Latitudo $9^{\circ} 45'$ na $10^{\circ} 45'$ Kusini mwa Ikweta na Longitudo $39^{\circ} 45'$ na $39^{\circ} 50'$ Mashariki. Kwa upande wa Mashariki Manispaa ya Lindi inapakana na Bahari ya Hindi na pande zote zilizobaki imezungukwa na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi.

*Kiutawala Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ina Jimbo 01 la Uchaguzi ambalo ni Jimbo la **LINDI MJINI**. Manispaa hii ina Tarafa Tatu (3), Kata 20 na Mitaa 117. Ina Madiwani 27 kati ya hao 20 wa kuchaguliwa na 7 wa kuteuliwa.*

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwezi Agosti, mwaka 2012 Halmashauri ya Manispaa ina watu wapatao 78,841 ikiwa Wanawake ni 41,316 na Wanaume ni 37,525.

Shughuli kuu za kiuchumi kwa wakazi wa Manispaa ya Lindi ni Kilimo kwa asilimia 80, na mazao ya Chakula yalimwayo ni Mpunga, Mahindi, Muhogo, MBAAZI, Kunde na Mtama na Mazao ya biashara ni Korosho, Ufuta na Nazi. Pia wapo Wafanyabiashara wachache na shughuli za Uvuvi kwa wananchi waishio kando kando ya Bahari ya Hindi.

Hali ya Ulinzi na Usalama katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ni ya kuridhisha. Pamoja na uhaba mkubwa wa vitendea kazi uliopo katika Jeshi la Polisi, Jeshi hilo limejipanga vyema kukabiliana na kudhibiti hali yoyote ya uvunjaji wa sheria kwani hakuna matukio makubwa ya uvunjaji wa amani japokuwa kuna matukio madogo madogo ambayo hujitokeza na kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

4.0 ORODHA YA MIRADI YA MWENGE – 2017

Mwenge wa Uhuru 2017 katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi utakimbizwa Umbali wa KM 162 ambapo utaweka Mawe ya msingi Miradi 02, Utafungua Miradi 02, Utazindua Miradi 02 na Kutembelea Miradi 03 na hivyo kufanya Jumla ya Miradi 09 itakayopitiwa na Msafara wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2017. Miradi hiyo ina thamani ya **Tsh 2,905,679,038** kama inavyoonesha katika jedwali lifuatalo:-

| N A | JINA LA MRADI | GHARAMA ZA MRADI | KAZI YA MWENGE | KATA | IDARA |
|----------------|--|-----------------------------|--|-----------------------|---------------------------|
| 1 | <i>Mradi wa upimaji Viwanja 2,090 Eneo la Ngongo na kukabidhi Hati kwa ajiri ya Ujenzi wa Viwanda katika Maeneo ya Ngurumahamba.</i> | 50,677,000 | <i>Kuweka Jiwe la Msingi na Kukabidhi Hati 3 za Viwanja kwa ajili ya Viwanda</i> | Jamhuri | <i>Mipangomiji</i> |
| 2 | <i>Mradi wa kukamua Mafuta ya Nazi (Tsh 24,605,0000 na Ufunguzi wa Ofisi ya Kata ya Ng'apa(Tsh 24,000,000)</i> | 48,605,000 | <i>Kuzindua Mradi wa kukamua Mafuta ya Nazi na kukagua umaliziaji wa Ofisi ya Kata.</i> | Ng'apa | <i>Kilimo / Viwanda</i> |
| 3 | <i>Mradi wa Matengenezo ya kawaida Barabara ya Mtutu-Cheleweni</i> | 429,297,080 | <i>Kuweka Jiwe la Msingi</i> | Ng'apa | <i>Ujenzi</i> |
| 4 | <i>Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Nandambi</i> | 78,242,000 | <i>Kufungua Mradi</i> | <i>Tandango ngoro</i> | <i>Afya</i> |
| 5 | <i>Mradi wa Shamba la Choroko</i> | 1,930,000 | <i>kutembelea</i> | Chikonji | <i>Kilimo</i> |
| 6 | <i>Mradi wa Maji Chikonji</i> | 1,970,901,548 | <i>Kuweka Jiwe la Msingi</i> | Chikonji | <i>Maji</i> |
| 7 | <i>Mradi wa Madarasa 3 katika Shule ya Sekondari Mkonge.</i> | 85,913,490 | <i>Kufungua Mradi</i> | <i>Msinjahili</i> | <i>Elimu</i> |
| 8 | <i>Mradi ya Vikundi vya Ushonaji vya Vijana na Wanawake vilivyowezeshwa kupitia 10% ya Makusanyo ya ndani ya Manispaa</i> | 201,112,920 | <i>Mwenge kukabidhi Hundu za mikopo kwa Vikundi na kuona shughuli zinazofanywa na vikundi hivyo.</i> | Makonde | <i>Maendeleo ya Jamii</i> |
| 9 | <i>Mradi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa shughuli za Afya (GoT – MIS)</i> | 39,000,000 | <i>Kuzindua Mradi.</i> | Makonde | <i>Tehama</i> |
| JUMLA | | 2,905,679,038 | | | |

**MCHANGANUO WA GHARAMA ZA KILA MRADI UTAKAOTEMBELEWA NA MWENGE
WA UHURU MWAKA 2017 KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI.**

| NA | JINA LA MRADI | GHARAMA ZA MRADI | | | | KAZI YA MWENGE |
|--------------|--|----------------------|--------------------|-------------------|----------------------|--|
| | | SERIKALI KUU | HALMASHAURI | WANANCHI | JUMLA | |
| 1 | <i>Mradi wa upimaji Viwanja 2,090 Eneo la Ngongo na kukabidhi Hati kwa ajiri ya Ujenzi wa Viwanda katika Maeneo ya Ngurumahamba.</i> | 0 | 50,677,000 | 0 | 50,677,000 | <i>Kuweka Jiwe la Msingi na Kukabidhi Hati 3 za Viwanja kwa ajili ya Viwanda</i> |
| 2 | <i>Mradi wa kukamua Mafuta ya Nazi (Tsh 24,605,000 na kuona umaliziaji wa Ofisi ya Kata ya Ng'apa(Tsh 24,000,000)</i> | 0 | 24,000,000 | 24,605,000 | 48,605,000 | <i>Kuzindua Mradi wa kukamua Mafuta ya Nazi na kukagua umaliziaji wa Ofisi ya Kata.</i> |
| 3 | <i>Mradi wa Matengenezo ya kawaida Barabara ya Mtutu-Cheleweni</i> | 429,297,080 | 0 | 0 | 429,297,080 | <i>Kuweka Jiwe la Msingi</i> |
| 4 | <i>Mradi wa Ujenzi wa Zahanati ya Nandambi</i> | 44,000,000 | 15,000,000 | 19,242,000 | 78,242,000 | <i>Kufungua Mradi</i> |
| 5 | <i>Mradi wa Shamba la Choroko</i> | 0 | 0 | 1,930,000 | 1,930,000 | <i>Kutembelea Mradi</i> |
| 6 | <i>Mradi wa Maji Chikonji</i> | 1,970,901,548 | 0 | 0 | 1,970,901,548 | <i>Kuweka Jiwe la Msingi</i> |
| 7 | <i>Mradi wa Madarasa 3 katika Shule ya Sekondari Mkonge.</i> | 0 | 85,913,490 | 0 | 85,913,490 | <i>Kufungua Mradi</i> |
| 8 | <i>Miradi ya Vikundi vya Ushonaji vya Vijana na Wanawake vilivoyezeshwa kupitia 10% ya Makusanyo ya ndani ya Manispaa</i> | 114,586,919.6 | 80,000,000 | 6,526,000 | 201,112,920 | <i>Mwenge kukabidhi Hundi za mikopo kwa Vikundi na kuona shughuli zinazofanywa na vikundi hivyo.</i> |
| 9 | <i>Mradi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa shughuli za Afya (GoT – MIS)</i> | 24,000,000 | 15,000,000 | 0 | 39,000,000 | <i>Kuzindua Mfumo, kugawa kadi za CHF na kuona ukarabati wa kituo.</i> |
| JUMLA | | 2,582,785,549 | 270,590,490 | 52,303,000 | 2,905,679,038 | |

4.1 TAARIFAYA MRADI WA UPIMAJI VIWANJA MAENEKO YA NGONGO NA NGURUMAHAMBA

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, kutokana na kasi ya ukuaji wa Mji wa Lindi na kupanuka kwa shughuli za kijamii na kiuchumi, imepelekea ongezeko kubwa la uhitaji wa viwanja kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwekezaji wa viwanda vidogo na vikubwa.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Sera ya ardhi ya mwaka 1995 imeeleza bayana kwa kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga maeneo maalum kwa ajili ya viwanda na uwekezaji pamoja na kutenga maeneo kwa matumizi mbalimbali kulingana na mahali na uwekezaji. Manispaa ya Lindi tunatekeleza Sera hii kwa vitendo.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Katika kutekeleza kaulimbiu ya Mwenge mwaka huu isemayo ‘**Shiriki Kukuza Uchumi wa Viwanda kwa Maendeleo ya Nchi Yetu**’ Halmashauri ya Manispaa ya Lindi imepima viwanja 2,090 kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo Viwanda. Upimaji huu umegharimu jumla ya **Tsh. 50,677,000**


Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi imetenga eneo la viwanda vidogo na vikubwa katika maeneo ya Ngurumahamba na tayari viwanja kwa ajili ya viwanda vitatu vya **Kubangua Korosho, kutengeneza Magunia, na Kutengeneza dawa ya Unga aina ya Salfa (Sulphur)** vimepimwa na leo utakabidhi Hati 3 za maeneo haya ili ujenzi wa viwanda hivyo uanze mara moja.

Nduqu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Faida za mradi huu ni pamoja na:

1. Kudhibiti ujenzi holela wa makazi hususan katika maeneo ya Ngongo.
 2. Kuongeza hadhi ya viwanja vya Maonesho ya NaneNane kwa kusogezza huduma mbalimbali za kijamii kama maji, umeme, barabara, shule na afya.
 3. Mapato ya Manispaa na Serikali kuu yataongezeka kutokana na uuzaaji wa viwanja na mapato endelevu yatokanayo na kodi ya Ardhi na Majengo.
 4. Ongezeko la ajira kwa wananchi wa Manispaa na Mkoa wa Lindi kwa ujumla
 5. Viwanda vitakavyojengwa vitarahisisha upatikanaji wa soko la mazao.
 6. Viwanda hivi vitakuwa chachu ya ujenzi wa viwanda vingine vikubwa na videoqo katika kushiriki kukuza uchumi wa viwanda.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, Baada ya taarifa hii fupi, kwa heshima na taadhima sasa tunakuomba Utuwekee jiwe la msingi katika mradi wetu huu wa upimaji wa viwanja eneo la Ngongo na kisha ukabidhi Hati Miliki tatu (3) za ardhi kwa **Bodi ya Korosho Tanzania**, ambaye ni Mwekezaji wa kiwanda cha Kutengneza Magunia, Kubangua Korosho na Kutengeneza Dawa ya Unga (sulphur) vitakavyojenqwa eneo la Ngurumahamba.

MWENGE OEEEEEE..... "SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA NCHI YETU" MWENGE OEEE



ENEO LA VIWANJA VYA NGONGO NA NGURUMAHAMBA

4.2 TAARIFA YA KIKUNDI CHA USINDIKAJI WA MAFUTA MWALI YA NAZI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Kikundi chetu kinaitwa **JIKOMBOE**. Kikundi kilianzishwa mwezi Agosti mwaka 2011 kikiwa na idadi ya wanachama 18, wanaume walikuwa 6 na wanawake 12. Kutokana na sababu mbalimbali, wanakundi wengine walijitoa kundini na sasa tumbaki wanachama 10, wanaume 2 na wanawake 8. Kikundi chetu kimesajiliwa rasmi na tumeshafungua akaunti katika benki ya NMB.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Kikundi hiki kilanza kujishughulisha na usindikaji wa zao la nazi mwezi Agosti mwaka 2014 kwa lengo la kuongeza thamani ya zao ili kujiongezea kipato. Mashine yetu ina uwezo wa kukamua mafuta kwa asilimia 60, yaani kiasi cha nazi 20 hadi 25. Kiasi hiki cha Nazi kina uwezo wa kuzalisha Lita 1 ya mafuta ambayo inauzwa kwa bei ya **Tsh. 20,000** kwa sasa.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Kikundi hiki kimefadhiwa na kituo cha utafiti wa zao la nazi Mikocheni Dar es Salaam. Watafiti hawa walikuja na kuhamasisha uundaji wa vikundi vya usindikaji mafuta mwali ya nazi ili kuongeza thamani ya nazi. Walitoa mafunzo na kuelezea dhana nzima ya usindikaji mafuta mwali pamoja na kuwapatia wanakikundi mashine ya mkono ya kukamulia mafuta yenyе thamani ya shilingi 3,000,000/=.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Kikundi kilipatiwa mkopo wa Tsh. 200,000
kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ambapo tayari tumeshalipa mkopo wote
na tumepeatiwa mkopo mwengine wa Tsh 1,000,000 na leo tunatarajia utatukabidhi
Hundi hivo ikiwa ni miongoni mwa hundi 4 utakazokabidhi leo.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Kikundi chetu kinakumbana na changamoto nyinai katika utekelezaji wa kazi zake. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:

1. Mtaji mdogo kwa ajili ya uendeshaji wa kikundi
 2. Kikundi kukosa Ofisi ya kudumu.
 3. Uwezo mdogo wa machine kukamua mafuta yanayotosheleza Soko.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Ili kukabiliana na changamoto tulizotaja hapo juu, sisi wanakikundi tumejipanga na kudhamiria kufanya yafuatayo:

1. *Kwenda taasisi za kifedha kwa ajili ya kukopa kwa lengo la kuongeza mtaji.*
 2. *Kikundi kina mpango wa kununua eneo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi.*
 3. *Kushiriana na shirika la SIDO kuongeza tija kwa kutumia mashine bora zaidi.*
 4. *Kuendelea kushiriki maonyesho mbali mbali ili kujifunza kutoka kwa wengine na kujitangaza zaidi.*

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Baada ya taarifa hii fupi, kwa heshima na taadhima sasa tunakuomba utuzindulie Mradi wetu wa kusindika mafuta mwali ya Nazi, Ukabidhi hundi kisha uone jinsi tunavyofanya shughuli zetu, uone bidhaa ambazo tayari zimeshasindikwa na vikundi vyetu na mwisho ukague umaliziaji wa ujenzi wa Ofisi yetu ya Kata.



KIKUNDI CHA KUKAMUA MAFUTA YA NAZI - KATA YA NG'APA

4.3 TAARIFA MATENGENEZO YA BARABARA YA MTUTU-CHELEWENI (KM 18)

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Awali ya yote tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa kukubali kwako kufika hapa kwa lengo la kutuzindulia matengenezo ya barabara ya **Mtutu – Chelweni** yenye urefu wa **km 18**. Hii ni barabara moja kati ya nyingi zinazoendelea kufanyiwa matengenezo ndani ya Manispaa yetu ya Lindi kwa mwaka huu ambapo kwa pamoja zina urefu wa jumla ya Kilometra.....

Ndugu kiaonzi wa mbio za mwenge, Barabara ya Mtutu- Cheleweni inarahisisha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii katika kata nne (4) za Manispaa ya Lindi ambazo ni Ng'apa, Tandangongoro, Mtanda na Chikonji zenyе jumla ya wakazi 11,577.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Matengenezo ya barabara hii yanafanyika kupitia mfuko wa barabara “Road Fund” kwa kuwatumia wakandarasi wawili **M/s. Besta Holdings Company Ltd.** anayefanya matengenezo ya muda maalum ya **km 10.0** kwa gharama ya **Tsh 315,087,080** na **M/s. Nyagama Investment Ltd** anaye imarisha sehemu korofit **km 8.0** kwa gharama ya **Tsh 114,210,000**, hivyo matengenezo ya Barabara nzima hadi kukamilika yatagharimu **Tsh 429,297,080**. Matengenezo haya yanatarajiwa kukamilika kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Baada ya maelezo hayo mafupi, kwa heshima na taadhima tunakuomba sasa utuzindulie mradi huu wa matengenezo ya barabara ya Mtutu- Cheleweni yenyeye urefu wa km 18.0.

Mwenge Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeee.....!



MATENGENEZO YA BARABARA YA MTUTU - CHELEWENI

4.4 TAARIFA YA UJENZI WA ZAHANATI YA NANDAMBI.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mradi wa ujenzi wa Zahanati hii uliibuliwa na wananchi mwaka 2014 kufuatia usumbufu wanaoupata pale wanapohitaji huduma za Afya. Waathirika wakubwa katika tatizo hili wamekuwa ni akina Mama wajawazito na Watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Hadi kufikia hapa ujenzi huu umegharimu kiasi cha **Tsh 78,242,000**. Katika fedha hizi mchango wa wananchi ni **Tsh 19,242,000** zilizotokana na fedha za utunzaji wa Misitu. Halmashauri ya Manispaa ya Lindi imechangia **Tsh 15,000,000** na **Tsh 44,000,000** ni ruzuku ya maendeleo kutoa Serikali kuu.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Kukamilika kwa mradi huu kutawarahisishia wananchi wa Nandambi na vijiji jirani kupata Huduma za Afya kwa karibu kuliko ilivyo sasa hasa kina Mama wajawazito na watoto chini ya Miaka mitano na hatimae kupunquza vifo vya akina mama wajawazito na watoto.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, katika jitihada za kutokomeza ugonjwa wa Malaria hasa kwa akina mama wajawazito na Walemau, Halmashauri ya Manispaa imeandaa Vyandarua ambavyo utayakabidhi makundi haya muhimu ili wajikinge dhidi ya mbu waenezao Malaria.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2017, Baada ya kukusomea Taarifa hii fupi, kwa heshima na Taadhima tunaomba utuzindulie Jengo letu la Zahanati ya Nandambi Manispaa ya Lindi ili lianze kutumika kisha ukabidhi Vyandarua kwa makundi ya kina mama na Walemauvu.

Mwenge Oyeeeeeeeeeeeeeee.....!



PICHA YA ZAHANATI YA MTAALI WA NANDAMBI

4.5 TAARIFA YA MRADI WA SHAMBA LA CHOROKO - CHIKONJI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mradi huu wa shamba la choroko upo katika Mitaa ya Chikonji kaskazini na Chikonji Kusini. Mradi huu umeanza mwaka huu 2017. Shamba hili ni mali ya familia ya Ndugu **Mshamu Kassim Ally.**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Lengo la mradi huu ni kuongeza kipato kwa familia na jamii kwa jumla kwa Kijiji cha Chikonji na Manispaa ya Lindi kwa ujumla wake. Choroko sio zao linalolimwa kwa wingi katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, hivyo ni matumaini yetu kuwa wakulima wa Manispaa ya Lindi watajifunza mambo mengi kuhusiana na zao la choroko kupitia shamba hili. Zao la choroko ni zao la biashara katika Halmashauri hii Hivyo basi kwa kuongeza uzalishaji wa zao la choroko katika Halmashauri, kutasaidia kuboresha maisha ya wananchi.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Eneo hili la mradi lenye ukubwa wa ekari saba (7) limegharimu jumla ya **Tsh. 1,930,000** ikiwa ni asilimia 100 ya mchango wa familia. Katika msimu huu tunatarajia kuvuna jumla ya kilo 3150 ambapo kwa bei ya kawaida ni Tsh 800.00 kwa kilo na hivyo kufanya jumla ya **Tsh 2,520,000** zitakazopatikana. Tunatoa shukrani kwa wataalam wa Kilimo wa Manispaa kwa kutupatia ushauri wa kitaalamu na kanuni bora za kilimo.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mradi wetu bado unakabiliwa na changamoto nydingi ikiwa ni pamoja na:

- *Kukosekana kwa soko la uhakika na bei ya choroko kutokuwa na msimamo.*
 - *Mtaji mdogo kwa ajili ya kuboresha shamba ili kuongeza mavuno.*
 - *Uqumu wa masharti ya mikopo kutoka taasisi za fedha.*

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, Katika kukabiliana na changamoto hizo, tunaiomba Serikali na Wadau wengine wa Kilimo kutusaidia ili kilimo chetu kiweze kuwa na tija kwa maendeleo yetu na maendeleo ya taifa kwa ujumla. Baada ya kukusomea taarifa hii fupi Kwa heshima na Taadhima karibu ukague na kuona shamba yetu hili la Choroko.

Mwenge Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee.....!



SHAMBA LA CHOROKO – CHIKONJI

4.6 TAARIFA YA MRADI WA MAJI CHIKONJI

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, tunayo furaha kubwa kukukaribisha mwenge wa uhuru pamoja na ujumbe wake katika Kata yetu ya Chikonji. tunayo imani na matarajio makubwa kwa ujio huu kwani unatufungulia historia mpya baada ya kuhangaika kwa muda mrefu kutafuta Maji safi na salama.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, mradi wa maji **Chikonji** ni mmoja kati ya miradi saba (7) ya Maji iliyotekelizwa chini ya Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira (WSDP). Miradi mingine ilishakamilika na inaendelea kutoa huduma ya Maji katika maeneo ya **Kineng'ene, Tulieni, Kitumbikwela, Mingoyo, Mtange na Likotwa**.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mradi wa maji **Chikonji** umegawanyika katika mafungu matatu (3) ambayo ni:

1. Ujenzi wa visima katika vyanzo vya Maji na miundombinu ya usambazaji wa maji maeneo ya **Chikonji Kusini na Kaskazini**.
2. Ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji maeneo ya **Jangwani na Nanyanje**
3. Ujenzi wa miundo mbinu ya kusambaza maji katika maeneo ya **Mkanga**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, mradi huu una kandarasi tatu, nazo ni:

1. **Shanxi Construction Engineering Corporation & Minerals Company** kwa gharama ya **Tshs 1,171,919,650.00**
2. **Gemtech Investment Company Limited** kwa gharama ya **Tshs 315,261,408.00 na**
3. **YN Investment Company Limited** kwa gharama ya **Tshs 483,720,490.00**

kampuni zote zikiwa za Dar Es salaam. Kazi hizi zote zinafanywa kwa usimamizi wa Kampuni ya **Don Consult Limited ya Dar Es Salaam** ambapo Mradi huu hadi kukamilika kwake utagharimu kiasi cha Shilingi **1,970,901,548.00**.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mradi huu utakapokamilika utawanufaisha wakazi zaidi ya **7,800** wanaoishi katika mitaa ya **Kiwanjani, Koleji, Likabuku, Nanjinga, Mkanga, Nanyanje, Jangwani na maeneo yanayozunguka mitaa hiyo**. Mradi huu utakuwa na uwezo wa kuzalisha lita **175,000** kwa siku. Hii itamaliza tatizo la upatikanaji wa Maji kwa 100% kwa wakazi wa mitaa yote ya Kata ya Chikonji na maeneo yanayoizunguka.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mpaka kufikia leo hii utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia **90** na Wakandarasi wote wapo wanaendelea kumalizia kazi chache zilizosalia. Tunatarajia hadi kufikia tarehe 30 Juni 2017 mradi utakuwa umekamilika na wananchi tutaanza kupata maji safi na salama.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, Kwa niaba ya wananchi wa Manispaa ya Lindi, sisi wakazi wa Chikonji tunaishukuru Serikali yetu kwa kuwezesha utekelezaji wa mradi huu kwani utaongeza chachu ya maendeleo kwa kupunguza muda wa kutafuta maji hasa kwa kina mama. Pia tunakushukuru wewe binafsi kwa kuja katika mradi wetu kwani kupitia mwenge umehamasisha maendeleo siyo katika sekta ya maji tu, bali hata sekta zingine zote kwa ujumla.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, Baada ya kusikiliza taarifa ya mradi wetu, sasa kwa heshima na taadhima tunakuomba utuwekee jiwe la msingi.

Mwenge Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeeee.....!



MRADI WA MAJI CHIKONJI

4.7 TAARIFA YA UJENZI WA MADARASA 3 SHULE YA SEKONDARI MKONGE

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Shule ya sekondari ya Mkonge ni shule ya kutwa ya wavulana na wasichana yenye jumla ya wanafunzi 560. Shule hii ina jumla ya vyumba 12 vya madarasa na vyumba 3 vya maabara na hivyo kuwa na upungufu wa vyumba 3 vya madarasa.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Ili kuondoa changamoto hii ya upungufu wa vyumba vya madarasa, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi imejenga vyumba 3 vipyta vya madarasa ambavyo vimegharimu kiasi cha tsh **85,913,490 pamoja na VAT**. Ujenzi wa vyumba hivi vya madarasa ulianza Mwezi Disemba 2016 na kukamilika mwezi April 2017.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, ili kuunga mkono jitihada za kuboresha miundombinu ya Elimu katika Shule za Sekondari, **Mhe, Hamida Mussa Abdallah Mbunge Viti maalum Mkoa wa Lindi aliahidi kuchangia mifuko 100 ya Saruji** na leo atakukabidhi Saruji hiyo ili umkabidhi Mkuu wetu wa Wilaya kwa ajili ya utekelezaji.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Kufunguliwa kwa madarasa haya kutaondoa kero ya mlundikano wa wanafunzi madarasani na hivyo walimu kuwa na nafasi ya kutosha ya kupita na kukagua nukuu pamoja mazoezi ya wanafunzi wakati wa vipindi.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Baada ya kuwasilisha taarifa hii fupi, kwa heshima na taadhima tunaomba sasa utufungulie vyumba hivi 3 vya madarasa, Upokee mifuko 100 ya Saruji na mwisho ushuhudie jitihada za Wanafunzi kuhusiana na mapambano dhidi ya UKIMWI, Malaria na Madawa ya kulevya kupitia michezo waliyoandaa.

Mwenge Oyeeeeeeeeeeeeeee.....!



MADARASA 3 SHULE YA SEKONDARI MKONGE

4.8 TAARIFA YA ASILIMIA 10 YA VIKUNDI YA WANAWAKE NA VIJANA

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Awali ya yote tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa kukubali kuona shughuli mbalimbali zinazofanywa na wanavikundi saba vya ushonaji ambavyo ni: Majani Mapana, Msonobarini Juu, Sheikh Badi, Mikumbi Magharibi, Kota, Majengo na Ndoro chini. Jumla ya watu katika vikundi hivi ni 67 ikiwa wanaume ni 10 na wanawake ni 57.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mradi huu uliibuliwa mwaka 2012 kwa Lengo la kuwawezesha Vijana wasio na ajira kupata zana za kisasa za ushonaji, chini ya ufadhili wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Uamzi huu umekuwa chachu ya kuongeza hamasa kwa vijana kujiajiri katika fani ya ushonaji.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Serikali kupitia TASAF imetuwezesha kiasi cha **Shilingi milioni mia moja kumi na nne, mia tano themanini na sita elfu, mia tisa kumi na tisa (114,586,919.60)**. Sisi wanakikundi tumechangia **Shilingi milioni sita, mia tano ishirini na sita elfu, (6,526,000/=)** kupitia nguvu kazi. Fedha hizo zilituwezesha kununua Cherehani 12 za kawaida, Mashine 52 za kudarizi, Mashine 6 za “Overlock”, Mashine 6 za kufuma maua, Vifaa mbalimbali vya ushonaji pamoja na kujenga ofisi kwa ajili ya vikundi vyetu.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Matarajio yetu katika mradi wetu huu ni:

1. Kuongezeka kwa kipato kwa kila mwanakikundi katika vikundi hivi sita (6),
2. Ongezeko la vijana kuingia katika fani hii ili wapate ujuzi hatimaye wajiajiri.
3. Kupata mikopo kutoka Taasisi za kifedha kwa ajili ya kuijendezeza.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi inaendelea kutekeleza maelekezo ya serikali ya kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani, kwa ajili ya kuviwezesha Kiuchumi vikundi vya Wanawake na Vijana. Kwakufanya hivi inatekeleza kwa vitendo Sheria ya bajeti iliyopitishwa na Bunge mwaka 2015.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Manispaa ya Lindi imetua kiasi cha shilingi Milioni 80 (80,000,000) kwa **Chama cha akiba na mikopo cha ILULU (ILULU SACCOs)** kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake na vijana. Katika zoezi hilo, Vikundi 37 vya Wanawake na 36 vya Vijana vitanufaika na mkopo wa shilingi milioni Moja (1,000,000) kila kikundi na hivyo kufanya jumla ya shilingi milioni 73 zitakazokopeshwa.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, Katika Manispaa yetu ya Lindi pia tunapata mikopo kupitia Mfuko wa Rais wa Kujitegemea. Kwa mwaka 2016/2017 jumla ya Tsh

37,200,000 zimetolewa kupitia mfuko huo ambapo jumla ya vikundi 18 vya Wanawake na Vijana vimenufaika na mikopo hiyo.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, Halmashauri inathamini utoaji wa mikopo kwetu sisi Vikundi vya Wanawake na Vijana ili kuchochea juhudzi zetu katika kukuza uchumi na kuharakisha maendeleo ya nchi kwa ujumla. Tunaishukuru Serikali kuu na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kwa kutupatia fedha zilizotuwezesha kufikia hatua hii tuliyonayo leo.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge, Baada ya kusikia taarifa yetu, kwa heshima na taadhima sasa tunakuoamba ukabidhi hundi za mikopo kwa vikundi vilivypopo mbele yako vinavyowakilisha vikundi vingine ambavyo vimekidhi vigezo kasha utembelee banda letu ili ujionee matunda ya kazi zetu.



MRADI WA VIKUNDI VYA USHONAJI WAILES MAJANI MAPANA

**4.9 TAARIFA YA MFUMO WA KIELEKTRONIKI KATIKA KITUO CHA AFYA
MANISPAA YA LINDI**

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Karibu sana katika kituo chetu cha Afya cha Manispaa. Ukiwa hapa kituoni utazindua Mfumo wa kieletroniki wa kusimamia shughuli na huduma za sekta ya afya, utakagua ukarabati wa kituo unaoendelea na kisha utatoa kadi za **CHF** kwa watu 16 wanaoishi na Virusi vya **UKIMWI**. Shughuli zote hizi zimegharimu **Tsh 39,000,000**. Kati ya hizo **Tsh. 15,000,000** zimetolewa na Halmashauri na **Tsh 24,000,000** ni ruzuku ya maendeleo.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Mfumo wa kieletroniki wa kusimamia shughuli na huduma za Afya kwenye Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati umeanzishwa kwa lengo la kuboresha huduma za Afya na mfumo wa taarifa kwa njia ya mtandao na kuongeza tija katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na huduma za Afya.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Hadi sasa mfumo huu umekamilika na umegharimu kiasi cha **Tsh 15,000,000** zilizotolewa na Halmashauri ya Manispaa kutoka katika mapato yake ya ndani. Shughuli zilizofanyika hadi sasa ni pamoja na:

- i. Uwekaji wa Miundombinu ya Mtandao Kiambo (Local Area Network) katika vyumba vya madaktari, Chumba cha dawa, Mapokezi na maabara.
- ii. Kuendesha Mafunzo elekezi kwa madaktari na Wauguzi watakaotumia mfumo katika kutoa huduma.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Faida zitakazotokana na matumizi ya mfumo huu ni pamoja na:

- i. Utunzaji mzuri wa taarifa za wagonjwa wanaofika kituoni
- ii. Kuratibu mapokezi na ugawaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vidogo vinavyopokea dawa na vifaa tiba kutoka kituo hiki.
- iii. Kuratibu utoaji wa madawa kwa wagonjwa wanaohudumiwa hapa.
- iv. Kuratibu malipo ya huduma kwa wagonjwa wanaopata huduma kwa mpango wa kuchangia gharama (cost sharing).
- v. Kuwezesha mawasiliano kwa njia ya mtandao kwa watoa huduma katika maeneo tofauti anayopitia mgonjwa ndani ya kituo.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Katika kuhakikisha tunaongeza ufanisi na kutoa huduma zenye tija, Halmashauri iliamua kufanya ukarabati wa miundombinu ya Kituo hiki cha Afya. Hadi sasa jumla ya **Tsh 24,000,000** zimeshatolewa na Serikali kuu kupitia ruzuku ya maendeleo. Kazi ya ukarabati inaendelea vizuri na leo hii utakagua maendeleo yake.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Katika kuunga mkono jitihada za Serikali za Mapambano dhidi ya **UKIMWI** Halmashauri ya Manispaa imeandaa Kadi za **CHF** kwa ajili ya watu 16 wanaoishi na Virusi vya **UKIMWI**. Kadi hizi zitawawezesha kupata huduma na tiba kwa magonjwa nyemelezi wakati wote. Wenzetu hawa

watakaopata kadi hizi, wamejitokeza kwa hiari yao na wako tayari kushirikiana na jamii katika kutoa elimu kwa wengine.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge, Baada ya maelezo haya, kwa heshima na taadhima sasa tunakuomba kwanza utuzindulie mfumo huu wa kieletroniki, pili ukague ukarabati wa kituo unaoendelea na mwisho ukabidhi kadi za CHF kwa wenzetu wanaoishi na Virusi nya UKIMWI.

Mwenge Oyeeeeeeeeeeeeeeeeeee!



MWENGE OIEEEE..... “SHIRIKI KUKUZA UCHUMI WA VIWANDA KWA MAENDELEO YA NICHI YETU”..... MWENGE OIEEEEE

MFUMO WA KIELEKTRONIKI KATIKA KITUO CHA AFYA MANISPAA YA LINDI